

Kunahitajika nini ili kujiunga na NDIS?

Mpango wa Bima ya Taifa ya Ulemavu Australia ya Magharibi unaitwa kwa Kiingereza kwa kifupi (NDIS katika WA) ni njia mpya ya kuwasiadi watu wenye ulemavu kupata huduma na msaada kulingana na mahitaji yao ya sasa na siku za baadaye. Mpango huu unasimamiwa katika mahali husika WA na Idara ya Jamii – Huduma za Walemavu (iliyojulikana hapo awali kama Tume la Huduma za Ulemavu).

Mchakato unaofuatia unaonyesha hatua zinazofuatiwa kabla ya mtu kustahili kupokea huduma zinazofadhiliwa na mpango wa NDIS.

1. Kuhakikisha kama Unastahili

- Wasiliana na NDIS katika WA ili uhakikishe kama unastahili na kuomba msaada kwa NDIS.
- Piga simu nambari, 1800 996 214 au tembelea Ofisi ya Uratibu wa Mitaa.
- Utapokea majibu ndani ya siku, 21 za kalenda kutoka siku ulipowakilisha fomu za kuhakikisha ustahili wako wa Mpango.

2. Kuanzisha Mpango

- Ustahili unapokubalika, Mratibu wa Mitaa atakutana nawe kuanzisha mpango wako wa Mpango wa Bima ya Taifa ya Ulemavu.
- Mchakato wa mipango unaweza kuchukua hadi siku 90.

3. Tafuta Watoa Huduma

- Wakati wa kufanya mipango, Mratibu wako wa Mitaa atakusaidia kuchagua baadhi ya huduma za jamii, huduma za serikali na mashirika mengineo yanaytoa msaada.
- Mratibu wako wa Mitaa atakuuliza uwasiliane na wanaotoa hizi huduma wale ambao wanauwezo wa kukusaidia kutimiza malengo ya mpango wako.

**Kujiunga
na
NDIS**

4. Kukamilisha Mpango

- Huduma zako zinazofadhiliwa zitahitaji kupitishwa kabla ya kuwekwa kwa mpango wako wa NDIS.
- Huduma kawaida huanza kati ya wiki, 4-6 baada ya mpango wako kupitishwa.
- NDIS huendelea kwa kipindi cha mwaka 1, pasipokua vinginevyo maalum.

Tukiungwa Mkono na Idara ya Jamii (Huduma za Ulemavu)